# MAMBO 9 UNAYOTAKIWA KUJUA KUHUSU KUNENA

# KWA LUGHA

## Na jinsi unavyoweza kuanza kunena kwa lugha

## YALIYOMO

**SEHEMU YA KWANZA** .............................................................................................. 10

kunena kwa lugha ni nini?. ........................................................................................10

kuna aina mbili za kunena kwa lugha ...........................................................................14

1) lugha inayoelewa ila haifahamiki na msemaji...................................................................14

2) lugha isiyoeleweka na binadamu ..............................................................................16

kuna kunena kwa lugha kama huduma na kuna kunena kwa lugha kwa ajili ya kila mkristo..19

1) kunena kwa lugha kama huduma ..............................................................................21

2) kunena kwa lugha kwa kawaida ................................................................................23

kuna kusema kwa lugha hadharani na kusema kwa lugha binafsi...............................................27

kuna kusema kwa lugha, kuomba kwa lugha na kuimba kwa lugha............................................30

1) kusema kwa lugha .................................................................................................30

2) kuomba kwa kunena kwa lugha ...............................................................................31

3) kuimba kwa lugha ..................................................................................................32

je kunena kwa lugha kumekoma?...............................................................................34

je kunena kwa lugha ni kwa shetani? ..........................................................................37

nina hutubu kwa hiyo sina haja ya kunena kwa lugha..............................................................40

je kila mkristo anaweza kunena kwa lugha ........................................................................45

kunena kwa lugha ni kwa wapentekoste au walokole au watu wa rohoni sana..........................50

1) je kunena kwa ni kwa wapentekoste au walokole.............................................................50

2) je kunena kwa lugha ni kwa watu wa rohoni........................................................................51

**SEHEMU YA PILI**............................................................................................... 53

kuna faida gani ya kunena kwa lugha..........................................................................53

1) kunena kwa lugha kunakujenga wewe kama mkristo.........................................................59

2) kuombea kitu ambacho hukijui au hujui uombe vipi.........................................................64

3) kunena kwa lugha ni njia ya kutoa shukrani.......................................................................67

4) kunena kwa lugha ni njia ya mungu kuzungumza na wewe.............................................68

**SEHEMU YA TATU** ........................................................................................................ 70

mambo mengine unayohitaji kuyajua kuhusu kunena kwa lugha .........................................70

1) roho mtakatifu sio anayenena kwa lugha ..............................................................70

2) neno moja au maneno mengi ......................................................................................72

3) imani vs hisia ....................................................................................................................73

4) je kila mkristo lazima anene kwa lugha, au kama sineni kwa lugha ina maana mimi sio mkristo..........................................................................................................................75

5) kunena kimya kimya au kwa sauti kubwa.................................................................76

je na mimi ninaweza kunena kwa lugha? .......................................................................7 7

## VITABU VINGINE VYA MWANDISHI

### CHRISTIAN

1) How God taught me prosperity part 1
2) How God taught me prosperity part 2

### NON- CHRISTIAN

1) UTT AMIS kwa mtu mwenye haraka
2) Jinsi ya kuweka katika soko la hisa
3) Jinsi ya kuwekeza katika hati fungani

**©Maombi A. Chagamba**

**Simu: +255713999596,**

**+255752102169**

**WhatsApp:**

**+255713999596**

**Email wiseinvestorr@gmail.com**

# UTANGULIZI

Kuna sababu 3 ambazo zinafanya wakristo wengi wasinene kwa lugha nazo ni

1)Kunena kwa lugha kumekoma

Kuna baadhi ya watu wamefundishwa ya kwamba kunena kwa lugha kumekoma, katika kitabu hiki nitakufundisha kuwa hili sio kweli

2) Sio kila mtu anaweza kunena kwa lugha

Kitu kingine ambacho kinafanya wakristo wasinene kwa lugha ni kuwa kuna watu ambao wanafundisha kuwa sio kila mtu anaweza kunena kwa lugha bali kunena kwa lugha ni kwa baadhi ya wakristo na hii nitakuonyesha kimaandiko kuwa sio kweli

3) Kutojua umuhimu wa kunena kwa lugha

Kuna baadhi ya watu hata kama wanajua ya kuwa kila mkristo anaweza kunena kwa lugha na ya kuwa kunena kwa lugha hakujakoma, hawajui umuhimu wa kunena kwa lugha.

**STORY**

Miaka mingi kidogo iliyopita (mwanzoni wa mika 1900) mzee mmoja (mmarekani) alikuwa na binti yake ambaye alikuwa mmisionari (missionary) afrika, huyu binti alikuwa ameolewa na yeye pamoja na mume wake walikuwa wamisionari, sasa kama utakuwa umesoma historia kidogo wamisionari wengi walikuwa wanapoteza maisha kutokana na magonjwa ambayo walikuwa wanakutana nayo pindi ambapo wanakuwa afrika, sasa kulikuwa na ugonjwa ambao ukikutana nao enzi hizi basi wewe ndio umekwenda, kulikuwa hakuna kinga wala tiba, ukionekana na huo ugonjwa basi ndugu na jamaa wanachofanya ni kuandaa mazingira ya namna ya kukuzika na kama utataka kuchagua nyimbo kwa ajili ya mazishi yako basi inabidi uchague mapema kwani hakuna uwezakano wa kupona, sasa huyu binti alipokuwa afrika akapatwa na huu ugonjwa , na kama unakumbuka enzi hizi hakukuwa na simu wala mawasiliano yoyote kutoka afrika kwenda marekani ambayo yangefikisha taarifa haraka, sasa akiwa hoi na amepoteza fahamu akiwa kwenye hatua za mwisho za kupoteza uhai, baba yake ambaye alikuwa marekani akaamka siku hiyo ili aendelee na shughuli zake (alikuwa mfugaji), akaamka asubuhi kwa ajili ya kulisha kuku,ng’ombe na nguruwe, ila siku hiyo alipoamka akahisi katika roho yake kuna kitu hakiko sawa, alikuwa na ushuhuda kuwa binti yake aliyeko afrika maisha yake yako hatarini, akaacha kazi ya kulisha wanyama akaenda pembeni na kuanza kuomba, kwa kuwa alikuwa hajui tatizo la binti yake lilikuwa ni nini, akaamua kuomba kwa kunena kwa lugha, ilikuwa takribani saa 3 asubububi, mkewe alipoamka

akamkuta mumewe anaomba akaamua asimsumbue akaendelea kuandaa chai ya asubuhi, mzee akaendelea kuomba saa la kwanza likakatika,saa la pili,la tatu , mkewe kila akija kumuangalia anakuta mzee bado amepiga goti anaomba kwa lugha tu, ikatoka asubuhi ikaja mchana  mzee bado hajaondoka, upande wa pili kuku,nguruwe na ng'ombe wanapiga kelele njaa, toka asubuhi hawajaletewa kitu, ilipofika mchana mke wa mzee akaamua kuandaa chakula cha mchana, mzee akaendelea kuomba kwa lugha mpaka saa nane, ilipofika saa nane roho yake ikapata amani ya kuwa alichokuwa anakiombea kimemalizika akaanza kucheka kwani roho yake inamshuhudia ushindi akaendelea kwenda kulisha nguruwe, kuku na ng'ombe ambao wakati huu walikuwa wamesha hesabu siku hiyo mzee amewalazimisha kufunga kwa kuomba na wao.(joking)

Sasa baada ya muda binti yake aliyekuwa afrika akarudi marekani na mzee akakaa na binti yake na mkwe wake akawauliza, hivi tarehe Fulani majira kama haya ulikuwa na tatizo gani? Binti akaanza kumuelezea ya kuwa siku hiyo muda kama saa nane (baada ya kukaribisha tofauti ya majira) nilikuwa nimepoteza fahamu kwa ugonjwa ambao hauna tiba ila kwa miujiza ilipofika saa nane fahamu zikanirudia na nikiwa mzima kabisa bila dalili za ugonjwa wowote, kama unakumbuka ni majira ya saa nane mchana ndio mzee alihisi ushindi wa alichokuwa anakiombea.

Mungu yuko serious (makini) kuliko binadamu, hakuweka kipawa cha kunena kwa lugha kwa sababu alikuwa amekosa maneno ya kujaza biblia, bali aliweka

kipawa cha kunena kwa lugha kwa ajili ya kutusaidia kwa ajili ya maisha yetu ya kikristo.

Chukulia mzee wetu hapo juu alikuwa hafahamu namna ya kunena kwa lugha au kuitikia kile ambacho alikuwa anashuhudiwa na roho yake kufanya nini unadhani kingetokea? Yamkini angempoteza binti yake lakini ashukuliwe Mungu aliyeweka karama ya kunena kwa lugha katika maisha ya kikristo.

Biblia inasema

**Romans 8:26a**

*Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo*

Moja kati ya namna ambazo Roho anatusaidia kuomba ipasavyo ni kwa kupitia kunena kwa lugha, yamkini ungekuwa unanena kwa lugha kuna baadhi ya ndugu,au vitu usingeweza kuvipoteza au kuna baadhi ya vitu ambavyo ungevipata katika maisha yako kama ungekuwa unafahamu kunena kwa lugha.

Katika kitabu hiki nitakufundisha ya kuwa kunena kwa lugha ni kwa kila mkristo na ya kuwa kunena kwa lugha hakujakoma na kukuonyesha umuhimu wa kwa nini ukitaka kukua kiroho na kutembea na Mungu kwa viwango vya juu kunena kwa lugha ni moja ya kitu ambacho ni lazima.

# SEHEMU YA KWANZA

## KUNENA KWA LUGHA NI NINI?.

Unaweza kuwa umesikia neno kunena kunena kwa lugha au umesikia mtu akinena kwa lugha ila ukawa huelewi kunena kwa lugha ni nini au umeoona mtu ananena kwa lugha ila ukawa hujui nini anafanya, biblia ina mengi ya kusema juu ya suala la kunena kwa lugha.

Yesu kabla hajaondoka baada ya ufufuo wake aliwapa maagizo wanafunzi wake ya kuwa wakahubiri injili kwa kila kiumbe na akasema kuwa watu watakao amini watakuwa na ishara zifuatazo.

**Marko 16:17-18**

*Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo;*

***watasema kwa lugha mpya;***

*Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

Yesu mwenyewe ndio alisema ya kuwa wale watakao amini watakuwa na uwezo wa kunena kwa lugha mpya, sasa anacho maanisha hapa sio kwamba ukiwa mkristo kama ulikuwa haufahamu kiingeleza basi utaanza kuongea kiingeleza au kifaransa (ijapokuwa inawezekana tutaona hapo mbele ) ila alichokuwa

anakizungumzia hapa ni kuwa wale waaminio watakuwa na uwezo wa kuzungumza lugha ambayo hawajajifunza kwa uwezo wa Roho mtakatifu na hii lugha ambayo watazungumza iko ya namna mbili (tutaona hapo mbele, kwenye aina za lugha)

**Matendo ya mitume 1:8-9**

*Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*

*Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao.*

Hii ni siku ambayo Yesu alikuwa anapaa kuelekea mbinguni baada ya ufufuo na akawaambia wanafunzi wake wasubiri yerusalemu mpaka watakapopokea ahadi ya baba ambayo ilikuwa Roho mtakatifu, na baada ya Yesu kuwa amepaa wanafunzi wake wakabaki yerusalem wakisubiri ahadi ya Roho mtakatifu na baada ya siku kumi baada ya Yesu kuwa amepaa mbinguni Roho mtakatifu akawashukia.

**Matendo ya mitume 2:1-5**

*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja.*
*Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.*
*Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao.*
*Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, **wakaanza kusema kwa lugha nyingine**, kama Roho alivyowajalia kutamka.*
*Na walikuwako Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.*

Kama utakumbuka katika kitabu cha Marko tumeona ya kuwa Yesu alitaja ishara tano ambazo zitafuatana na wale ambao wanaamini na moja kati ya ishara ni kusema kwa lugha mpya na hapa tumeona ya kuwa baada ya Roho mtakatifu kuja juu ya wanafunzi wa Yesu ambao walikuwa 120 wakaanza kusema kwa lugha mpya KAMA ROHO ALIVYOWAJALIA KUTAMKA.

Hii ndio mara ya kwanza inarekodiwa katika maandiko ya kuwa watu wamenena kwa lugha, kunena kwa lugha ndio karama pekee ya Roho mtakatifu ambao haipo katika gano la kale ukiangalia karama zote ambazo zimeorodhesha katika kitabu cha wakorintho wa kwanza zote zinaonekana katika agano la kale isipokuwa kunena kwa lugha

Kunena kwa lugha ni karama pekee ambayo ni mpya na ipo agano jipya pekee sasa kama Mungu ameona kuiweka katika kanisa basi ina maana ni kitu cha muhimu.

**Simu: +255713999596,**

**+255752102169**

**WhatsApp:**

**+255713999596**

**Email [wiseinvestorr@gmail.com](mailto:wiseinvestorr@gmail.com)**

PATA NAKALA NZIMA YA KITABU KWA KUWASILIANA NA MWANDISHI

